



Habari  
Jumataha April 7  
2026

## Wafariki ajali ikihusisha lori

MPUMALANGA, Afrika  
Kusini

**W**ANAWAKE wanne wamefariki dunia kutokana na ajali ya barabara iliyo husisha gari ndogo na lori katika Jimbo la Mpumalanga, Afrika Kusini.

Ajali hiyo ilitokea kwenye Barabara ya R23 kati ya Volksrust na Perdekop baada ya magari hayo kugongana uso kwa uso.

Kwa mujibu wa taarifa za mamlaka, wanawake hao waliopoteza maisha walikuwa abiria ndani ya gari ndogo iliyo husika katika ajali hiyo.

Watu wengine wanne, akiwemo dereva wa gari hilo pamoja na abiria watatu, walijeruhiwa na wote walikimbizwa hospitali ya karibu iliyopo Standerton kwa ajili ya matibabu.

Akizungumza kuhusu tukio hilo, Msemaji wa Idara ya Usalama wa Jamii, Usalama na Uhusiano wa Mpumalanga, Mandla Chauke alisema chanzo cha ajali kinachunguzwa ingawa kuna uwezekano wa uzembe katika uendeshaji.

Waziri wa Usalama wa Jamii, Usalama na Uhusiano wa jimbo hilo (MEC), Jackie Macie alituma salamu za rambirambi kwa familia zilizopoteza wapendwa wao na kuwatakiya nafuu ya haraka majeruhi.

Aidha, Macie alitoa wito kwa madereva kuzingatia sheria za barabarani na kuendesha kwa umakini ili kupunguza ajali.

Aliongeza kuwa barabara ya R23 ni miongoni mwa barabara zenye msongamano mkubwa wa magari hususani wakati wa sikukuu na mapumziko, hali inayochangia kuongezeka kwa ajali katika eneo hilo.